Karama za Roho na Huduma

“Mungu huwakirimia washiriki wote wa kanisa lake katika kila kizazi karama za kiroho ambazo kila mshiriki atatumia katika huduma ya upendo kwa ajili ya ustawi wa wote kanisani na wa wanadamu. Zikitolewa kwa nguvu za Roho Mtakatifu, ambaye humgawia kila mshiriki kama apendavyo Yeye, karama hizi hutoa uwezo wote na huduma zinazohitajika na kanisa katika kutimiza kazi iliyoagizwa kimbingu. Kulingana na Maandiko Matakatifu, karama hizi ni pamoja na huduma kama vile imani, kuponya, unabii, kuhubiri, kufundisha, utawala, upatanisho, huruma, na huduma ya kujinyima na upendano wa kusaidia na faraja kwa watu. Baadhi ya washiriki wameitwa na Mungu na kukirimiwa na Roho kwa ajili ya shughuli zinazotambuliwa na kanisa katika uchungaji, uinjilisti, utume na huduma ya kkufundisha inayohitajika hasa katika kuwapa zana washiriki kwa ajili ya huduma, kulijenga kanisa hata likomae kiroho, na kukuza umoja wa imani na kumjua Mungu. Wakati washiriki wanapozitumia karama hizi za Roho kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za Mungu, kanisa hulindwa dhidi ya mivuto ya uharibifu wa mafundisho ya uwongo, na hukua kwa ukuzi utokao kwa Mungu, na kujengwa imara katika imani na upendo.” (Rum.12:4-8; 1Kor.12:11-11, 27, 28; Efe.4:8, 11-16; Mdo.6:1-7; 1Tim.3:1-3; 1Pet.4:10, 11)

Maneno aliyosema Yesu kabla ya kupaa mbinguni yangebadili historia. “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe” (Mk.16:15). Ulimwenguni mwote…? Kwa kila kiumbe…? Wanafunzi wangefikiri kuwa ni kazi isiyowezekana. Kristo hali akijua hali yao kuwa hawajiwezi, aliagiza wasitoke Yerusalemu bali waingoje “ahadi ya Baba”. Ndipo alipowahakikishia kuwa “mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi.” (Mdo.1:4, 8). Baada ya Yesu kupaa, wanafunzi walitumia muda mwingi kwa maombi. Umoja na unyenyekevu vilichukua nafasi ya kutofautiana na wivu vilivyotia doa wakati wao wakiwa na Yesu. Wanafunzi walikuwa wameongoka. Uhusiano wao karibu na Yesu na umoja uliotokea, vilikuwa muhimu kwa kujazwa Roho Mtakatifu. Kama Kristo alivyotiwa mafuta na Roho Mtakatifu afanye utume wake (Mdo.10:38), wanafunzi nao walipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu (Mdo.1:5) kuwawezesha kushuhudia. Siku waliyopokea Roho Mtakatifu, walibatiza watu elfu tatu. (Angalia Mdo.2:41).

Karama za Roho Mtakatifu

Kristo alifafanua karama za Roho Mtakatifu kwa mfano. “Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri.” (Mt.25:14, 15).Mtu anayesafiri kwenda mbali inamwakilisha Kristo. Watumishi wa mtu ni wafuasi wake ambao “wamenunuliwa kwa thamani” (1Kor.6;20)- “damu ya thamani ya Kristo (1:Pet.1:19).

Yesu amewakomboa ili watumike na “hawako hai tena kwa kwa ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa anjili yake Yeye aliyekufa akafufuka kwa ajili yao.” (2Kor.5:15). Kristo ametoa mema kwa kila mtumishi kwa kadiri ya uwezo wake na kila mtu “kazi yake” (Mk.13:34). Pamoja na karama na uwezo mbalimbali, mema haya huwasilisha karama maluum zinazotolewa na Roho Mtakatifu. Kwa maana maalum, Kristo aligawa karama hizi kanisani siku ya Pentekoste. “Alipopaa juu… aliwapa wanadamu vipawa” . Hivyo “kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. (Efe.4:7, 8).

Roho Mtakatifu ndiye Mtendaji, “akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye” (1Kor.12:11).

Makusudi ya Karama za Kiroho
Roho Mtakatifu humpatia uwezo wa kipekee mshiriki, na kumwezesha kulisaidia kanisa litimize utume wake.

Umoja ndani ya Kanisa. Kanisa la Korintho halikupungukiwa karama yoyote (1Kor.1:4, 7). Ila washiriki wake walitofautiana na kugombana kama watoto kuwa ni karama ipi iliyo muhimu kuliko nyingine. Kufuatia migawanyiko ndani ya kanisa, Paulo aliwandikia asili halisi ya karama hizi. Karama za kiroho, ni karama za neema. Kutoka kwa Roho mmoja, huja "tofauti za karama" ambazo huleta "tofauti za huduma" na "tofauti za kutenda kazi". Lakini Paulo anasisitiza kuwa ni "Mungu yeye yule azitendaye kazi zote katika wote" (1Kor. ambazo huleta "tofauti za huduma" na "tofauti za kutenda kazi". Lakini Paulo anasisitiza kuwa ni "Mungu yeye yule azitendaye kazi zote katika wote" (1Kor.12:4-6).

1. Jinsi zitendavyo kazi. Paulo anatumia mwili wa mwanadamu kuelezea umoja katika tofauti za karama. Mwili una viungo vingi, ambavyo kila kimoja huchangia ustawi wake. "Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alviyotaka." Hakuna kiungo kinachoweza kukiambia kiungo kingine, "sina haja na wewe". "Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa vinyonge zaidi, vyahitajiwa zaidi. Vile viungo vidhaniwavyo havina heshima, viungo vile twavipa heshima zaidi; na viungo vyetu visvyo na uzuri, vina uzuri zaidi. (1Kor.12:21-24). Viungo vilivyo vinyonge huhitaji ulinzi maalum. Twaweza kutembea pasipo mkono au mguu, lakini hatuwezi kutembea pasipo mapafu, maini au moyo. Huwa tunatoa nyuso na mikono yetu watu waone, lakini viungo vingine tunavisitiri kwa mavazi. Mungu anakusudia kwamba mgawanyo wa karama za roho kuzuia faraka na kuleta roho ya kuungana na kutunzana. Kama kiungo kimoja kikiugua, viungo vyote vitauugua navyo, na kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho. (1Kor.12;25, 26). Baada ya kuziorodhesha karama, Paulo anahitimisha kwamba "Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kasha miujiza, kasha karama za kuponya wagonjwa na masaidiano, na maongozi na aina za lugha." (1Kor.12:28). Kwa sababu si kila mshiriki atakuwa na karama zote, tumeitwa kuzitaka karama zilizo kuu. (1Kor.12:31).

2. Kipimo muhimu. Karama za Roho hazitoshelezi zenyewe peke yake. Iko njia iliyo bora (1Kor.12:31). Karama za Roho zitapita Yesu atakaporudi mara ya pili. Tunda la Roho ni la kudumu milele. Tunda la Roho huja na hali bora ya upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema wote na haki na kweli ambavyo upendo huja navyo (Gal.5:22, 23; Efe.5:9). Unabii, kunena kwa lugha na ufahamu vitapotea, lakini imani, tumaini na upendo vitadumu, na lililo kubwa katika hayo ni upendo. (1Kor.13:13).

Upendo huu ambao Mungu hutoa (kwa Kigiriki agape), ni upendo unaojinyima na kutoa upendo kwa kitu au mtu anayependwa, upendo ambao hukua kutokana na heshima ya vilivyo bora vilivyomo ndani ya mtu/kitu. Karama zisizo na upendo huleta faraka na migogoro kanisani. Kwa hiyo njia bora ni kuufuata upendo, na kutaka sana karama za rohoni. (1Kor.14:1).

Kuishi kwa utukufu wa Mungu. Katika waraka kwa Warumi, Paulo anazungumzia karama za roho na kuwaita waumini wapate kuishi kwa utukufu wa Mungu (Rum.11:36 – 12:2). Anatumia kielelezo cha mwili kuonyesha utofauti wa viungo na huduma (fungu la 3-6). Katika sura ya 12, anaorodhesha: unabii, huduma, kufundisha, kuonya (kutia moyo), ukarimu, uongozi (usimamizi), na kurehemu. Kama katika Wakorintho, Paulo anamalizia kwa kanuni kuu ya upendo (fungu la 9). Petro anazungumzia karama za roho kwa kuangalia mwisho unaokaribia (1Pet.4:7). Umuhimu wake ni kuwa watu wazitumie karama kabla wakati haujaisha. Kila moja kadiri alivyopokea karama aitumie kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu (1Pet.4:10). Kama Paulo, anasema karama hizi siyo kwa kujivunia bali

kwa bali kwa utukufu wa Mungu (1Pet. 4:11). Pia alihusisha upendo na karama za roho. (1Pet.4:8).

Kukua kwa Kanisa. Paulo katika hoja yake ya tatu na ya mwisho kuhusiana na karama za roho, alisihi waumini kuishi maisha yanayostahili wito wao walioitiwa. Kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. (Efe.4:1-3). Karama za kiroho huchangia kuimarika kwa umoja ambao unasaidia Kanisa kukua. Kila mshiriki amepokea "neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo" (Efe.4: 7).

Kristo mwenyewe "alitoa wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, kata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo. (Efe. 4:11-13).

Huduma hizi huimarisha kanisa na kuliongezea uwezo wake wa kinga "ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujaja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo." (Efe.4:14, 15).

Hatimaye, katika Kristo, huduma hizi huleta umoja na ustawi wa kanisa. "Katika Yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo." (Efe. 4:16). Kukua huwa kwa aina mbili; kwanza; kuongezeka washiriki na kuongezeka kwa karama za kiroho kwa mshiriki moja moja. Tena, upendo ni sehemu ya wito, kwa kuwa kila mshiriki atatumia karama zake kwa upendo.

Athari za Karama za Kiroho

Huduma moja. Maandiko hayatetei wazo kwamba wachungaji wahudumu na washirki wapashe joto mabenchi wakisubiri kulishwa. Wote wachungaji na washiriki ni watu wa miliki ya Mungu (1Pet.2:9). Wote wameitwa kuutayarisha ulimwengu ili kumpokea mwokozi arudipo. (Mt.28:19, 20; Ufu.14:6-12).

Jukumu la Viongozi wa Kiroho. Fundisho la Karama za kiroho huweka jukumu la kufundisha washiriki kwa viongozi wa kiroho ili washiriki wafanye iliyo kazi yao. Mafanikio ya mpango wa Mungu kwa kanisa hutegemea utayari na uwezo wa wachungaji kuwafundisha washiriki kutumia talanta walizopewa na Mungu.

Karama na Utume. Mungu hutoa karama za kiroho kulifaidia mwili wote ambao ni kanisa na siyo tu mshiriki anayezipokea**.** Kadhalika kanisa halipokei karama kwa ajili yake tu ila kulisaidia kutimiza utume ambao Mungu amelipa.

Umoja katika kutofautiana. Baadhi ya wakristo hujaribu kuwafanya wengine wafane nao. Huo ni mtazamo wa kibinadamu wala siyo mpango wa Mungu. Karama zimetolewa tofauti tofauti kwa kufaidiana. Katika Kristo, jiwe kuu la pembeni, "jengo lote linaunganishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana." (Efe.2:21)

Kushuhudia - kusudi la karama. Waumini hupokea karama tofauti ni ishara kuwa kila moja ana huduma yake iliyo tofauti. Hata hivyo bado mshiriki anapaswa kuikiri imani yake

akishuhudia yale Mungu aliyomtendea. Makusudi ya karama kwa ujumla wake ni kumfanya mshiriki ashuhudie.

Kushindwa kutumia karama. Waumini ambao wanashindwa kutumia karama siyo tu kwamba karama zao zinapotea bali wanahatarisha fursa yao kuupata uzima wa milele. (Mt.25:26-30)

Kuzitambua Karama za Kiroho

Ili washiriki wafanikiwe kwenye utume wa Kanisa, wanapaswa kuzitambua karama zao. Kuzitambua karama za kiroho kwapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

Maandalizi ya Kiroho. Mitume waliomba kwa umakini ili wapate kufaa kusema Neno litakalowavuta wenye dhambi kwa Kristo.Waliondoa tofauti zao na matamanio yao ya kuwa wakubwa. Twapaswa kuendelea kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu tumsihi atupatie hekima kuzitambua karama tulizo nazo. (Yak.1:5)

Kujifunza Maandiko. Kujifunza Agano Jipya kwa maombi kutafanya akili zetu zitambue karama tulizonazo na tunazoweza kuzitumia kwa utukufu wa Mungu. Ni jukumu letu pia kuamini Mungu amempatia kila moja wetu angalau karama moja kwa utumishi wake.

Kuwa tayari kwa kile Mungu anachotupatia.Hatumtumii Roho bali ni Mungu ndiye atendaye kazi ndani yetu, “kutaka kwetu, na kutenda kwetu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.” (Filp.2:13).

Kuthibitishwa na Kanisa. Kwa kuwa Mungu ndiye atoaye karama kujenga kanisa lake, twaweza kutarajia hatimaye uthibitisho wa karama zetu kutokea kwenye maamuzi ya mwili wa Kristo wala siyo hisia zetu wenyewe.